*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 114-134*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.7

# Dhima za Tungo za Malezi katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Tenzi Teule

*Maryam Y. Mwinyi*[1] na *Shani Omari Mchepange*[2]

## Ikisiri

Malezi ni suala muhimu katika jamii na ni dhamira iliyowashughulisha wanafasihi mbalimbali, ikiwamo utenzi. Makala hii imechunguza dhana ya malezi katika tenzi teule ambazo ni: *Utenzi wa Mwanakupona*, *Howani Mwana Howani*, *Siraji* na *Utenzi wa Adili* kwa kuzingatia malengo manne mahususi. Makala imechunguza dhima za tenzi teule kifasihi, kijamii na kwa watunzi wenyewe. Nadharia za Sosholojia ya Fasihi na Mwingilianomatini zimeongoza uandishi wa makala hii. Data za makala zimekusanywa kwa kusoma matini teule na machapisho mengine yanayohusiana na mada hii. Matokeo yanaonesha kwamba watunzi husika wamefanana na kutofautiana katika kuzungumzia malezi. Kwa watunzi wa kike, dhima zilizojitokeza ni kumcha Mwenyezi Mungu, kujipamba na tabia njema, maisha ya ndoa, utii kwa wazazi, usafi na umaridadi pamoja na umuhimu wa elimu na kazi. Kwa watunzi wa kiume dhima zilizojitokeza ni utiifu na heshima, mapenzi na ndoa, bidii katika kazi, elimu ya kujitegemea, uvumilivu, uadilifu katika ushahidi, kutunza siri na kutimiza ahadi. Kwa watunzi wote wa kike na kiume, dhima zilizojitokeza kwa kufanana ni mazingatio ya muktadha wa jamii, nafasi ya baba na mama katika malezi na ukamilifu katika malezi.

## 1.0 Utangulizi

Utenzi ni miongoni mwa nui zinazoujenga utanzu wa ushairi, na kazi zake ni kuelimisha, kuadabisha, kuonya, kuburudisha na kuadilisha. Katika fasihi ya Kiswahili, kuna tenzi kadhaa za watunzi wanaume na wanawake, wakiwamo Muhammad Kijumwa na Mwanakupona Binti Mshamu. Wengine ni Shaaban Robert na Zaynab Himid, Mathias Mnyampala, Kulikoyela Kahigi, Kaluta Amri

[1] Mwalimu Mwandamizi Daraja C, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dodoma, Tanzania. Baruapepe: mayumwi@gmail.com

[2] Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, ChuoKikuu cha Dar es Salaam. Baruapepe: shaniom@yahoo.co.uk, shaniom@udsm.ac.tz

na Muhammed Khatib. Kwa pamoja, watunzi tajwa wameandika tenzi zenye dhamira tofauti wakisawiri kweli za maisha katika jamii. Moja ya dhamira muhimu zilizochomoza sana katika kazi za baadhi ya watunzi hawa ni malezi. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), malezi ni mafundisho, aghalabu mazuri, ya mzazi au mlezi katika makuzi ya mtoto. Pia, malezi hutazamwa kuwa ni njia ya uleaji na ukuzaji wa mtoto kwa kumfunza mienendo inayostahiki kufuatana na utamaduni wa jamii (TUKI, 2004; BAKIZA, 2010; Ndalu na Mirikau, 2014). Hivyo basi, nui ya tenzi ina nafasi kubwa katika kuelezea malezi, kwa maana ya maadili yanayobeba tunu au mambo yanayotakiwa katika jamii husika.

Kwa miaka kadhaa, kumekuwa na ongezeko la jitihada za watafiti, waandishi na wahakiki kuchunguza tenzi zinazozungumzia malezi kwa mitazamo na malengo tofauti. Kwa mfano, uhakiki wa *Utenzi wa Mwanakupona* uliofanywa na Khatib (1985) na Senkoro (1988) umegusia namna Mwanakupona alivyomlea binti yake kwa jicho la ukandamizaji. Pia, Njozi (1990) katika makala yake iitwayo *Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics*, ameuhakiki utenzi tajwa na kubaini kuwa Mwanakupona amemlea binti yake katika malezi ambayo kila mwanamke wa Kiislamu-Kiswahili anapaswa kupata. Aidha, kuna kazi kuhusu maisha na kazi za Muhammad Kijumwa ambazo ndani yake kuna utenzi wa *Siraji* uliohakikiwa na Egl (1983). Kazi nyingine ni kuhusu nafasi ya mwanamke katika tenzi mbili za Shaaban Robert iliyohakikiwa na Maina (2005). Pamoja na umuhimu wa jitihada hizo katika kukuza fasihi ya Kiswahili, hoja za waandishi hawa zinatofautiana katika mawanda na uchunguzi wa makala hii. Mathalani, kazi zao hazikujikita katika kuielezea dhamira ya malezi katika tenzi hizo kwa kuzingatia wakati na jinsi ya waandishi wake.

Vilevile, ulinganifu wa ujinsi wa baba na mama kwa malezi ya watoto haukuwekwa wazi katika kazi zilizotangulia. Aidha, uzingativu wa hadhi na itikadi za waandishi waliozungumzia malezi hauko wazi sana kwa wanagenzi wa fasihi ya Kiswahili kupata undani wa kilichokusudiwa katika kazi zilizotangulia. Kwa pamoja, maandiko yaliyotangulia yana udhaifu wa kutoangalia dhamira zinazofafanua dhana ya malezi kwa undani. Hivyo, ilikuwa muhimu kuchunguza kwa kulinganisha kufanana na kutofautiana baina ya watunzi wa kike katika dhima ya malezi Pia, tumechunguza kwa kulinganisha kufanana na kutofautiana baina ya watunzi wa kiume katika dhima ya malezi na dhamira zake. Kisha, tumelinganisha kufanana na kutofautiana watunzi wa kike na kiume. Aidha, tumechunguza dhima za tenzi teule kifasihi, kijamii na kwa watunzi wenyewe.

Kufikia malengo tajwa, makala hii imejikita katika kazi za Mwanakupona Binti Mshamu (*Utenzi wa Mwanakupona*, 1858), Zaynab Himid (*Howani Mwana Howani*, 2004), Muhammad Kijumwa (*Siraji*, 1927) na Shaaban Robert (*Utenzi wa Adili*, 1966). Sababu ya uteuzi huu ni kwamba, watunzi hawa wamezungumzia malezi ya watoto wa kike na wa kiume mtawalia. Aidha, kazi hizi zimeteuliwa

kwa sababu zimeangalia malezi ya watoto kwa jicho angavu na uzingativu wa mafanikio duniani na akhera. Aidha, tenzi hizi zimeteuliwa kwa sababu msingi wa hoja zake umefungamanisha malezi na imani ya kumridhisha Mola Muumba pamoja na kuwafanyia wema viumbe vyake. Halikadhalika, tenzi tajwa zimeonesha matakwa ya ndani ya waandishi wake katika kubainisha njia bora za malezi. Kwa mintarafu hii, tenzi hizi zimekuwa na upekee kutokana na kukwepa mtenguo na kupata unusura (Ponera, 2014).

Data za makala hii zimechambuliwa kwa kutumia Nadharia za Sosholojia ya Fasihi na Mwingilianomatini. Kwa mujibu wa Wellek na Warren (1978) Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi imeasisiwa na Mfaransa aliyeitwa Hippolyte Adolphe Taine (1828-1893). Msingi wa nadharia hii ni kusisitiza uhusiano baina ya kazi ya fasihi na mtunzi, asasi za jamii husika na muktadha uliopo. Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu imewasaidia watafiti kupata muongozo wa kuthibitisha jinsi tenzi teule zilivyoathiriwa na mazingira, jinsi na thamani ya hadhira lengwa (Wellek na Warren, 1978; Wamitila, 2003). Kwa upande mwingine, Nadharia ya Mwingilianomatini iliasisiwa na Julia Kristeva (1966). Msingi wake ni kwamba matini ya kifasihi ina mwingiliano na matini tangulizi. Yaani, hakuna matini inayojisimamia bila kuhusiana na matini nyingine. Nadharia hii iliteuliwa kwa sababu iliwasaidia watafiti kupata mwega wa kuelezea mahusiano ya kazi teule (Wamitila, 2003) zilizopishana zama (Kristeva, 1966). Kwa ujumla, nadharia hizi zimesaidia kuonesha muelekeo wa kutambua namna watunzi wanavyoyasawiri maisha katika jamii zao kwa jicho la kiudadisi.

Mapitio ya maandiko yalifanyika kati ya mwezi wa nne, 2015 hadi mwezi wa saba, 2017 kwa Mkabala wa Uhemenetiki. Kwa mujibu wa Boell na Cecez-Kecmanovich (2014), Mkabala wa Uhemenetiki hujumuisha utafutaji wa makala, upangaji na upaji sura wa dhana, uhakiki wa kina na ukuzaji au mwendelezo wa hoja. Mkabala huu ulitumika wakati wa kusoma majarida, vitabu, tasnifu na makala mbalimbali kuhusu malezi na ulitoa njia za kuthibitisha kinachojulikana na kubainisha kisichojulikana kwa mada teule. Hivyo basi, maneno kama vile malezi, wazazi, watoto, walezi na jamii yamezingatiwa ili kupata mtiririko wa maana. Utangulizi huu umefuatiwa na wasifu wa watunzi wa tenzi teule na kazi zao. Kisha, vimefuatia vipengele vya ulinganisho wa dhamira ya malezi ya watunzi wa kike na mjadala wake. Baadaye, ulinganisho wa dhamira ya malezi kwa watunzi wa kiume na mjadala wake kabla ya kufuata ulinganisho baina ya dhamira ya malezi ya watunzi wa kike na kiume pamoja na dhima za tenzi teule kifasihi, kijamii na watunzi wenyewe. Mwisho, limefuata hitimisho na mapendekezo ya makala.

## 2.0 Wasifu wa Watunzi Teule na Kazi zao

Kwa mnasaba wa makala hii, maelezo yafuatayo kuhusu wasifu wa watunzi na kazi zao ni muhimu katika kujenga hoja za uchambuzi wa tenzi teule.

### 2.1 Mwanakupona Binti Mshamu (1810/12-1860)

Huyu ni mwanamke mzaliwa wa Pate katika eneo la Siu nchini Kenya. Aliolewa na Bwana Mataka (rais wa Siu) na kuzaa naye watoto wawili, Mwanahashima na Muhammad Mataka. Mwanakupona alisikika na kuvuma sana katika viunga vya upwa wa Kenya hadi leo hii. Hii ni kwa sababu ya utenzi wake mashuhuri aliouita *Utenzi wa Mwanakupona* (1858). Inasemekana wanawake wa maeneo hayo wameuhifadhi vichwani utenzi huu na kuutongoa katika shughuli mbalimbali za dini kama vile ndoa, sherehe za harusi na matanga (El-Maawy, 2011). Aidha, inasadikiwa kuwa kuugua kwa mwaka mzima, hofu ya kuondoka duniani na kumwacha binti yake bila muongozo, ni miongoni mwa sababu za Mwanakupona kutunga utenzi huu (Njozi, 1990; Timammy na Swaleh, 2013). *Utenzi wa Mwanakupona* una beti 102 na ndio ulioandikwa, kwa maana kuwa tenzi zake nyingine kadhaa hazikuwahi kuandikwa (Njozi, 1990; Mulokozi, 1999 na El-Maawy, 2011).

### 2.2 Zaynab Himid (1918-2002)

Mwandishi huyu ni mshairi aliyepata umaarufu wa utunzi wa tungo mbalimbali akiwa mwalimu wa shule. Aliwahi kutunga tenzi, mashairi na michezo ya kuigiza. Baadhi ya kazi hizi walipewa wanafunzi kwa ajili ya kuigizwa na kusomwa kwenye sherehe mbalimbali katika visiwa vya Zanzibar na kwingineko. Mathalani, alitunga mchezo wa kuigiza ulioitwa "Unguja ya Leo sio ya ana" na shairi la kumsifu Mwalimu Nyerere aliloliita "Nyerere Rais Mwema, mwenye Busara na Hekima". Zaynab Binti Himid aliolewa vyuo vitatu (mara tatu). Hakujaaliwa kupata mtoto bali alilea watoto wa ndugu zake kama wa kwake mwenyewe (Othman na Yahya, 2004). Miongoni mwa mashairi yake ni tenzi za *Howani Mwana Howani* na *Mwana Kukuwa*. Kwa muktadha wa makala yetu, tumechunguza utenzi wa *Howani Mwana Howani* wenye beti 398. Kwa mujibu wa maelezo ya Zaynab (2004: viii) mambo mengi aliyoyaandika katika tenzi zake alihadithiwa na mama yake. Mambo mengine, alifanyiwa na mama yake alipokuwa mdogo na mengine mengi alimfundisha alipokuwa kigori hadi alipoolewa. Kwa pamoja, tumewatititirisha Mwanakupona na Zaynab kimpangilio kwa kuwa kazi zao zinawalenga watoto wa kike, jambo lililoongeza ubora wa data iliyokusudiwa (Cohen, Manion na Morrison, 2011). Aidha, tuliwateua hawa wawili kwa sababu kazi zao zina historia ya kusomwa na kujadiliwa katika majukwaa ya kifasihi, kiasi cha kutupatia fursa ya kuielewa kwa ukaribu dhana ya kuwalea watoto kwa jicho la amana kutoka kwa Mola Muumba.

### 2.3 Muhammad Kijumwa (1855-1943)

Huyu ni mtunzi maarufu wa mashairi na nyimbo katika visiwa vya Lamu nchini Kenya. Pia, alikuwa mchongaji mzuri wa hati za Kiarabu kwa kutumia mbao na

mawe. Hati hizo zilipachikwa kama nakshi kwenye milango na makaburi. Inasadikiwa kuwa Kijumwa alikuwa mwepesi wa kujibu bila ya kufikiri kama inavyothibitishwa katika baadhi ya beti zake (Abdulqadir[3], 2017). Kijumwa ameandika tenzi kadhaa ambazo hazijachapishwa. Miongoni mwazo ni *Utenzi wa Siraji* (1927) tulioukusudia katika makala hii. Katika utenzi huu, Kijumwa amemuusia mwanawe wa kiume aliyeitwa Helewa (Siraji), namna ya kutangamana na watu katika maisha. Tungo zake nyingine ni *Utenzi wa Mkunumbi* (1913), *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1913), *Alika kama Harusi* (kabla ya 1929), *Binti Yusufu* (1935), *Nasara wa Arab* (1936), *Utendi wa Safari* (1937) na *Wanawake wa Kiamu* (hm). Kijumwa alimuandikia *Utenzi Siraji*, baada ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kuonana na mwanawe huyo (Egl, 1983). Hivyo basi, walipoonana, Kijumwa alipata hamu ya kumwandikia yaliyomo ndani ya utenzi tajwa.

### 2.4 Shaaban Robert (1909-1962)

Shaaban Robert ni mwanafasihi aliyebobea katika uga wa tamthiliya, riwaya na ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa taarifa tulizozipata ndani ya kazi zake, Shaaban Robert ametunga diwani kadhaa za ushairi zikiwamo *Utenzi wa Vita vya Uhuru* (1939), *Almasi za Afrika* (1946), *Kielezo cha Fasili* (1959), *Pambo la Lugha* (1966) na *Mapenzi Bora* (1969). Pia, ametunga *Utenzi wa Adili* unaopatikana katika *Pambo la Lugha* (1966) na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1967). Taarifa zinaonesha kuwa baada ya kifo cha mkewe wa kwanza, Bi. Amina binti Kihere, aliyejaaliwa kupata naye watoto wawili Suleiman (Adili) na Mwanjaa; Shaaban Robert alitunga tenzi mbili, moja kwa kila mtoto ili ziwe mahala pa malezi ya mama. Sambamba na makala hii, tumeuchunguza *Utenzi wa Adili* wenye beti mia moja ili kuelewa malezi ya mtoto wa kiume bila ya mama. Chambilecho Waswahili, "likikosekana titi la mama hata la mbwa hufaa." Kwa ujumla, watunzi hawa wamezingatiwa katika makala hii kwa sababu kazi zao zimebeba utajiri wa mafunzo na ufasaha wa lugha iliyosadifu kuelezea malezi ya mtoto wa kiume.

## 3.0 Ulinganisho wa Dhamira ya Malezi Baina ya Watunzi wa Kike: Mwanakupona na Zaynab

Sambamba na lengo hili, ilikuwa muhimu kuwalinganisha Mwanakupona binti Mshamu na Zaynab Himid ili kufaidika na mitazamo ya watunzi hawa wanawake wa ukanda wa Pwani waliopishana kiumri na zama walizoishi. Katika ulinganisho huu, dhima za kumcha Mwenyezi Mungu, kujipamba na tabia njema, maisha ya ndoa, utii kwa wazazi, usafi na umaridadi pamoja na umuhimu wa elimu na kazi zimejitokeza. Kulinganishwa na kutofautishwa huko ni kama ifuatavyo:

[3] Huyu ni mtaalamu wa lugha ya Kiswahili na mbobezi wa ushairi kutoka Kisiwa cha Lamu aliyehojiwa na watafiti.

**3.1 Kumcha Mwenyezi Mungu**

Ni dhamira iliyozungumzwa na waandishi wote wawili katika tenzi zao. Wanasisitiza kuwa ili mwanaadamu aweze kuishi vizuri katika maisha ya dunia na baada ya kuondoka duniani, hana budi kumfuata Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza aliyoyaamrisha na kuacha aliyoyakataza. Hayo yatakamilika kwa kutimiza nguzo tano za Uislamu, nguzo sita za imani na kumtii mume kwa ukamilifu. Mwanakupona anamsisitiza binti yake kuwa Mcha Mungu kwa kufuata maamrisho ya mume, na Zaynab anahimiza utekelezaji wa nguzo tano kama ifuatavyo:

| | *Utenzi wa Mwanakupona* | | *Utenzi wa Howani Mwana Howani* |
|---|---|---|---|
| 12. | La kwanda kamata dini<br>Faradhi usiikhini<br>Na sunna ikimkini<br>Ni Wajibu kuitia | 193. | Shahada nguzo ya kwanza<br>Mtoto nikamfunza<br>Kusudi ni kumjuza<br>Nguzo tano kwa makini |
| 22. | Mama pulika maneno<br>Kiumbe ni radhi tano<br>Ndipo apate usono<br>Wa akhera na dunia | 196. | Nguzo ya pili mwanangu<br>Kuswali kumcha Mungu<br>Swala ina kubwa fungu<br>Thawabu ziso kifani |

Kimantiki, ujumbe wa beti hizi unaweza kutafasiriwa kuwa, msingi mkuu wa malezi ya watoto ni wazazi na walezi kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Muumba na Mlezi wa viumbe wote. Hapana shaka, ujumbe wa beti hizi unaweza kutumika katika muktadha wa Kiislamu na hata nje yake (Mwinyi, 2020). Kimsingi, wajuzi wa dini hawajivuni katika maisha ya dunia, na chambilecho Gibe (1993) na Sengo (1995), huaminika kwa kuiishi misingi ya dini yao.

**3.2 Kujipamba na Tabia Njema**

Hii ni dhamira nyingine ya malezi katika tenzi za *Mwanakupona* na *Howani Mwana Howani*. Wote wanawaelekeza watoto wao jinsi ya kujipamba na tabia njema na kuepuka tabia mbaya. Waliwahimiza binti zao kujiweka mbali na umbeya, dharau, uongo na tabia mbaya nyinginezo. Kwa undani, dhima za watunzi hawa zimejikita katika kuhimiza utangamano mzuri baina yao na viumbe wenzao. Hata hivyo, Zaynab anaonekana kwenda mbali zaidi kwa kueleza madhara ya tabia hizo. Mathalani, ametaja madhara ya zinaa, fitina, wizi na ulevi. Kwa upande wake, Mwanakupona hakulifanya hili. Yamkini, jamii katika zama za Mwanakupona hazikuwa na mwingiliano mkubwa na wageni na wigo wa vishawishi vya maasi haukulingana na nyakati za kina Zaynab. Beti zifuatazo zinafaa kuzingatiwa:

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 62. Sipende wenye jamali<br>Na utukufu wa maili<br>Fuqara ukamdhili<br>Cheo ukamvundiya | 359. Liko jengine la dhara<br>Ni huko kunywa Khamra<br>Maovu utapurura<br>Sijitie ulevini |
| 63. Akupendae mpende<br>Akuizao mwenende<br>Kwa zema mvundevunde<br>Laala akaridhia | 360. Ulevi waleta kila maovu<br>Maovu yenye muwala<br>Usingie hala hala<br>Ee! Mwana wa imani |

Yaliyomo katika beti hizi ni fikirishi na yanashawishi fikra kubwa kuchimba zaidi ili kuiona fikra kubwa ya malezi yenye kuzingatia ustawi mkubwa na ukamilifu. Mathalani, Mwanakupona anaonekana kuhimiza upendo kwa kuzingatia utu badala ya mali, jambo linalobeba mmoja wa misingi madhubuti ya tabia njema za wastaarabu (Sengo, 1995) waliofunzika (Sengo, 2007). Upevu wa ujumbe wa Zaynab nao si wa kubezwa. Husemwa pombe ni mama wa maasi. Pengine, ni kwa sababu ya sifa yake ya kuwatoa ufahamu walevi kiasi cha kuwa tayari kusema, kuimba, kucheka, na hata chambilecho El-Maawy (2011), kutembea ovyo nje bila ya udhuru wa maana.

### 3.3 Maisha ya Ndoa

Watunzi hawa wamezungumzia suala la ndoa kwa kiasi kikubwa. Chambilecho Zaynab, "mambo ya nyumba kunga makuti kuunga unga." Msisitizo wao mkubwa ni kuwa na maisha ya ndoa yenye kuzingatia mahusiano mema baina ya wahusika. Kwa upekee, Mwanakupona anaona raha ya maisha ya ndoa ni pale mke anapoweza kumdhibiti mume, kwa kumridhisha kwa kila alitakalo, kutomtia ghadhabu, kuomba ruhusa wakati wa kutoka, kumsinga na kutabasamu kila amuonapo. Zaynab kwa upande wake anahimiza mahusiano mema kwa kustahamiliana na kutunziana siri baina ya wanandoa hata majirani wasijue. Kwa mtazamo wake, mke ana hadhi ya umama katika ndoa. Baadhi ya beti zinazoakisi hayo ni hizi zifuatazo:

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 29. Enda naye kwa imani<br>Atakalo simkhini<br>We naye sikindaneni<br>Ukindani huumia | 266. Haya utapoolewa<br>Kichwani utachukuwa<br>Pengine utachopewa<br>Hakikutoshi jikoni |
| 31. Kilala siikukuse<br>Mwegeme umpapase<br>Na upepo asikose<br>Mtu wa kumpepeya | 269. Mwanamke huwa mama<br>Akatenda ya neema<br>Kiwa nazo darahima<br>Huendeleza nyumban |

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 50. Uonapo uso wake<br>Funuwa meno ucheke<br>Akwambialo lishike<br>**Ila kuasi jalia** | 270. Mambo ya nyumba ni kunga<br>Makuti kuunga unga<br>Wala sivyo kuifunga<br>Mwanangu mwana imani |

Katika beti hizi, kuna mengi ya kujifunza kwa ustawi wa ndoa. Funzo mojawapo linaweza kuwa ni mapenzi na utii baina ya wanandoa. Kwa mfano, Mwanakupona anasema, "we naye sikindaneni, ukindani huumia". Hapa, ni sawa na kusema kuwa maisha ya ndoa hayataki ushindani baina wanandoa husika, ili kuthibitisha taadhima yake kwa fahari kubwa (Gibbe, 1997). Kwa upande wa Zaynab, maelezo kuwa "mwanamke huwa mama" yana ujumbe mzito wa kuzingatiwa. Kimsingi, hujenga uthubutu wa kumpa mwanamke hadhi anayostahiki katika kuimarisha familia.

### 3.4 Utii kwa Wazazi

Watunzi hawa wameufungamanisha utii/heshima kwa wazazi, yaani baba na mama kuwa ni sababu ya kupata maisha bora duniani na akhera. Watunzi hawa wamehusisha pepo kwa watoto wasikivu kwa wazazi wao wenye kufuata maelekezo mema. Kimsingi, watunzi hawa wanabeba hoja kuwa mama ni mama katika hali yoyote aliyopo. Ufafanuzi wa haya umo katika beti zifuatazo:

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 7. Mwanangu twaa waadhi<br>Pamoya na yangu radhi<br>Mngu atakuhifadhi<br>Akuepue na baa | 376. Watii wazee wako<br>Wape mema matamko<br>Usikunje uso wako<br>Ukisemezwa nyumbani |
| 11. Yangu utakaposhika<br>Mwanagu hutosumbuka<br>Duniani utavuka<br>**Na akhira utakia** | 378. Jitahidi sana mama<br>Uwafurahishe mama<br>Kipata radhi zao mama<br>Utaingia peponi |

Beti hizi zimebeba ujumbe muhimu kuhusu kutii kwa kujua nafasi ya wazazi kwa mtoto. Watunzi hawa wamewapa wazazi nafasi ya ujenzi wa maisha na mustakabali mwema wa watoto wao. Jambo linalowawajibisha watoto kwa upande wao, kutii kikwelikweli (Shitemi, 2007) ili kupata mafanikio ya dunia na akhera (Kiango na Sengo, 1974).

### 3.5 Usafi na Umaridadi

Hii ni dhamira nyingine iliyomo katika tenzi za waandishi hawa. Usafi uliogusiwa ni wa aina mbili, usafi wa mwili (umaridadi) na wa nyumba. Mwanakupona anamtaka binti yake kuwa msafi na maridadi, anapokuwa nyumbani na iwe ni kwa ajili ya mumewe. Kwa upande wake, Zaynab anamueleza binti yake kuwa maridadi na kulinda utamaduni wa wanawake wa kizamani wa Kizanzibari. Yumkini lengo lilikuwa ni kuvuta haiba ya mwanamke kama inavyoelezwa katika baadhi ya beti zifuatavyo:

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 37. Mwanangu siwe mkoo<br>Tenda kama uonao<br>Kupea na kosha choo<br>Sidharau siku moya | 271. Nakufunza na zaidi<br>Mwana uwe maridadi<br>Uonekane jadidi<br>Kama watu wa zamani |
| 41. Pete sikose za ndani<br>Hina sikose nyaani<br>Wanda site matoni<br>Na nshini kuitia | 272. Karatasi za namna<br>Watu wakivaa sana<br>Nawe ujue kushona<br>Huvaliwa sikioni |

Katika beti hizi, mafunzo ya kujipamba na kujipodoa yamejitokeza. Yamkini, ni kwa lengo la kuendeleza mila na desturi za jamii ya Pwani ambayo ndiyo asili ya watunzi husika. Kwa mujibu wa Khamis (2016), mwanamke wa Pwani ana utamaduni wake wa kujipodoa na kujipamba kwa kutumia vitu mbalimbali kama vile mapambo ya fedha na dhahabu kwa sura ya vidani, pete, hereni, bangili na vikuku. Inaweza kusemwa kuwa, usafi na umaridadi ni kipengele muhimu katika maisha ya mwanamke wa Pwani. Kinyume cha mila na desturi hiyo ya usafi na umaridadi, jamii ya Pwani chambilecho Njozi (1990) na Sengo (2007) huanza kumdadisi mwanamke husika.

### 3.6 Umuhimu wa Elimu na Kazi

Dhamira hii imeguswa kwa jicho tofauti na watunzi hawa. Mathalani, Mwanakupona amejikita katika kumuelimisha binti yake kuhusu mbinu za kumdhibiti mume ili ajinasue na ubabe wake. Aidha, Mwanakupona amezungumzia kazi za ndani ya nyumba. Kwa kuwa Mwanakupona aliishi tabaka la waungwana, alimtaka mwanawe kuwa muongozaji tu wa kazi hizo na asiwe mshiriki kikamilifu. Kwa upande wake, Zaynab anamfundisha binti yake kujishughulisha na kazi za mikono za kiutamaduni wa Kizanzibari. Kwa elimu na ujuzi huu anaozungumzia Zaynab, alilenga kumsaidia binti yake ajisimamie endapo mumewe atamwachia kisichotosheleza, kama inavyooneshwa katika beti zifuatazo:

| *Utenzi wa Mwanakupona* | *Howani Mwana Howani* |
|---|---|
| 20. Sitangamane na watumwa<br>Ila mwida wa khuduma | 262. Hamfunza charahani<br>Apate kuwa mshoni |

| | |
|---|---|
| Watakuvutia tama | Akawa nambari wani |
| La buda nimekwambia | Kwao hao mtaani |

Kinachovutia katika beti hizi ni ujasiri wa watunzi wa kuthamini elimu na kazi kwa binti zao. Maelezo ya Zaynab yanaakisi dhana ya kujitegemea na kuondokana na utegemezi wa kiuchumi. Binti anapokuwa na elimu na ujuzi wa fani kama ya ushonaji na akaifanya kwa weledi, hapana shaka hupata msingi wa kujisimamia na kujipambanua kwa kujua anakotoka, alipo na anakokwenda (Sengo, 2012). Itoshe kusema kuwa aina hii ya mafunzo ya wazazi ni muhimu mno katika zama hususani za sasa zilizojaa pilikapilika na harakati za kujikomboa kiuchumi.

## 4.0 Mjadala wa Ulinganisho wa Dhamira ya Malezi ya Watunzi Teule wa Kike

Matokeo yamelingana pakubwa baina ya watunzi teule katika malezi ya mtoto wa kike. Yamkini, kulingana huko kumetokana na watunzi hawa kuwa waumini wa dini ya Kiislamu. Jambo hili, limewasaidia kufungamanisha malezi yao na mafunzo ya dini yao kwa kuhimiza utangamano mwema baina ya binadamu na Mola Muumba na binadamu na binadamu mwenzake katika jamii zao (Mwinyi, 2020). Hapa, kuna kusadifiana moja kwa moja kwa mafunzo yao na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ambayo kwa mujibu wa Wellek na Warren (1978) inaonesha uhusiano wa kazi za fasihi na muktadha wa jamii zinamoibukia. Kwa msingi huu, Watunzi hawa hawakuuacha Uislamu, Upwani, Uafrika pamoja na Uswahili wao katika kufikisha waliyokusudia (Sengo, 2012; Mwinyi, 2020) kwa kuakisi jamii zao. Hivyo, si ajabu kazi za watunzi hawa kuendelea kuishi miongoni mwa wanajamii husika. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa watunzi tajwa waliwalenga watoto wa kike pekee kwa kuwapa malezi ya kizamani. Kwa mujibu wa Mwinyi (2020), haya ni malezi yaliyojali utu, heshima, nidhamu na kuamiliana kwa wema baina ya wakubwa na wadogo.

Matokeo haya yanalingana na msingi wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaodai kwamba matini ya kifasihi ina mwingiliano na matini tangulizi. Kimantiki, ijapokuwa watunzi teule wameishi nyakati tofauti, bado maandishi ya Mwanakupona yanatoa mwega kwa Zaynab katika kuelezea mahusiano ya kazi (Wamitila, 2003) na jamii zao zilizopishana zama (Kristeva, 1966). Kwa msingi huu, inaweza kusemwa kwamba matini za watunzi teule, bado zinahitajika katika zama za sasa, hususani kwa jamii zinazokabiliana na mmomonyoko wa maadili (Sengo, 2007; Mwinyi, 2020). Hivyo, matini zitakazoandikwa sasa kuhusu malezi tayari zina mwega wa matini za watunzi teule. Fauka ya hayo, tofauti zilizojitokeza baina yao zinaweza kuhusianishwa na vipindi vya kihistoria vinavyopishana baina ya watunzi hao. Mathalani, usia wa Mwanakupona kwa binti

yake kutochanganyika na watumwa katika kazi, unaakisi zama za Umwinyi (Senkoro, 1988). Kinyume chake, malezi ya Zaynab yanaakisi jamii iliyo huru, yenye kuishi kwa ujamaa na kujitegemea. Kimantiki, matokeo haya yanapewa nguvu na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi inayotoa nafasi kubwa, kama wanavyosema Wellek na Warren (1978) kwa jamii kumuathiri mtunzi katika kazi yake.

## 5.0 Ulinganisho wa Dhamira ya Malezi baina ya Watunzi Teule wa Kiume

Sawa na lengo hili, watunzi Muhammad Kijumwa na Shaaban Robert wamelinganishwa. Kimsingi, watunzi hawa wamepishana kiumri na zama walizoishi. Kazi zao zimelinganishwa ili kufaidika na fikra, maono na mitazamo yao katika kusawiri maisha timilifu ya jamii. Katika ulinganisho huu, dhima za utiifu na heshima, mapenzi na ndoa, bidii katika kazi, elimu ya kujitegemea, uvumilivu, uadilifu katika ushahidi, kutunza siri na kutimiza ahadi zimejitokeza na kulinganishwa kama ifuatavyo:

## 5.1 Utiifu na Heshima

Watunzi husika wamewahimiza watoto wao kumtii Mola- Muumba kwa kufanya yaliyoamrishwa na kuacha yaliyokatazwa. Aidha, wanawahimiza watoto wao kumtegemea na kumuomba Mwenyezi Mungu Muumba na mmiliki wa vilivyomo duniani na akhera. Malipo yake ni pepo na kuokoka na adhabu za moto. Vilevile, watoto wamehimizwa kuheshimu wazazi na kuwaonywa kutowakemea, kutowakera na kutowadhalilisha. Msingi ni kwamba, wazazi ndio sababu ya wao kuwepo duniani na kupata baraka za Mwenyezi Mungu. Fauka ya hayo, watoto wametakiwa kuziheshimu mamlaka na viongozi wake, kuheshimu jamaa wa karibu, wakubwa na wadogo, matajiri na maskini. Kwa upekee, Shaaban Robert amemtaka Adili kumpa heshima mwalimu kwani ndiye mtoaji tongo za macho na kumpa mwangaza. Beti zifuatazo zinakidhi haja:

| *Utenzi wa Siraji* | *Utenzi wa Adili* |
|---|---|
| 5. Kwanda baba mcha Mungu<br>Utaokoka mwanangu,<br>Huku huko kwa utungu,<br>Kukosa cha kutumia | 10. Kwanza mche Mungu,<br>Mtengeza ulimwengu,<br>Juu akaweka mbingu,<br>Nyota zituangazie |
| 84. Mtii baba na mama,<br>Hata wakikusukuma,<br>Inyamaze yatakoma,<br>Simjibu ovu moya. | 36. Tatu baba na mama<br>Wataka taadhima<br>Na kila lililojema<br>Ukiweza watendee |

Beti hizi zinaonesha kwamba watunzi teule waliona haja ya kuweka msingi madhubhuti wa maisha yenye thamani. Kumcha Mwenyezi Mungu, kuwatii wazazi na kuwatendea wema ni wito adhimu katika malezi yenye tija. Matokeo yanaipa nguvu hoja ya Mbiti (2015), kuwa imani ya Mwenyezi Mungu ni msingi

madhubuti katika maisha. Kimantiki, watunzi teule wa kiume wanatoa hoja kuwa kuyafungamanisha maisha na imani kwa Mwenyezi Mungu na kuwaheshimu wazazi ni mtaji wa maisha tulivu usiokatika. Kwa upekee, Shaaban Robert katika ubeti wa 36 anaweka msisitizo kuwa wazazi nao ni binadamu kamili wanaohitaji kuheshimiwa. Kwa tabia hii njema, mtoto naye akikua ataheshimiwa na watu wengine katika jamii.

## 5.2 Mapenzi na Ndoa

Hii ni dhima nyingine ya malezi iliyoibuliwa na watunzi husika. Kijumwa anamtaka mwanawe ampende mkewe, ndugu na majirani kwa mapenzi ya kweli kwa kuwatatulia matatizo yao. Aidha, amemwelekeza mwanawe kuwa mkewe atakapodai talaka asifanye ajizi bali ampe na kisha akatafute mwingine. Aidha, alimgeukia binti yake na kumueleza kuwa mume atakapomwambia amwache basi afurahie na aihimize talaka. Kwa upande wake, Shaaban Robert anamtaka mwanawe aegemeze mapenzi yake zaidi kwa jamaa wa karibu, kuwasaidia wasonacho, mke na watoto wake. Zaidi, alimuonya kutowaamini watu wote. Beti zifuatazo zinaelezea hili:

| ***Utenzi wa Siraji*** | ***Utenzi wa Adili*** |
|---|---|
| 38. Nduzo wapende sana<br>Uteke ukiwaona<br>Iwapo hukutukana<br>Ifanye hukusikia | 59. Sita ukioa mke<br>Kwa mapenzi mshike<br>Simfanye makeke<br>Ila akuanze yeye |
| 174. Wetu binti sikia<br>Mwanamume kikwambia<br>Takuwata burahia<br>Akitinda nena haya | 76. Penda na watu wote<br>Aliye mbali mvute<br>Ila kuamini wote<br>Hili sana liambae |

Beti hizi zinaonesha kwamba watunzi wateule waliwafunza watoto wao busara ya kuishi kwa utulivu. Kimantiki, mtu hatarajiwi kuishi na kutenda kinyume cha mafunzo ya utu na heshima anayofunzwa na wazazi au jamii yake (Mwinyi, 2020). Matokeo haya yanakazia hoja ya Sengo na Kiango (1974) kwamba kuendelezwa kwa utu ndio kuendelezwa kwa mtu. Wazazi wanapoishi kwa kupendana, kuheshimiana na kujali utu wao hutoa fursa kwa watoto kujifunza zaidi. Huu ndiyo msisitizo mkubwa unaojitokeza kwa Shaaban Robert. Na kinyume chake ni sawasawa. Maelezo ya Kijumwa kwa binti kuwa "Mwanamume kikwambia, takuwata burahia, akitinda nena haya," yanathibitisha hoja hii. Hivyo basi, katika maisha ya ndoa kila mmoja ana wajibu wa kuimarisha mapenzi kwa ustawi wa familia.

**5.3 Bidii katika Kazi**

Watunzi wote wanawataka watoto wao kufanya kazi kwa bidii kwa sababu ndio msingi wa maendeleo. Aidha, kazi itawapa umaarufu na kuondoa umaskini. Pia, waliwataka watoto wao kujiepusha na uvivu wakati wote wa kutekeleza majukumu yao kazini. Hili linabainishwa katika beti zifuatazo:

| *Utenzi wa Siraji* | *Utenzi wa Adili* |
|---|---|
| 88. Na kazi fanya nadhifu<br>Utakuwa maarufu<br>Na ujira raufu<br>Na ukali kutotia | 90. Kazi yako idhibiti,<br>Ipe jicho la dhati,<br>Ukitoka katikati,<br>Wa’muzi jina wachie |

Ujumbe wa beti hizi ni kuwa maisha ni kazi. Kimantiki, mtu mwenye akili timamu na mzima wa afya hatarajiwi kukaa sawasawa bila ya kuwa na kazi ya halali ili kupata pato la kuzikabili gharama za kila siku na muhimu katika kulikabili jukumu la ulezi. Kwa mujibu wa Mdee, Njogu na Shafi (2011) kufanya kazi au kuishi kwa muda mrefu ndiko kunakompa mtu tajriba au uzoefu wa mambo katika jamii. Kwa maana hii, vijana watakapozingatia nafasi zao na kuyachukua mafunzo ya wazee wao, mafunzo ya watenzi teule yanatoa dira ya maendeleo kwa kufanya kazi.

**5.4 Elimu ya Kujitegemea**

Watunzi hawa walitambua umuhimu wa elimu ya kujitegemea. Hapa, waliwataka watoto wao kumakinikia elimu. Kwa upekee, Kijumwa amemhimiza mwanawe kuwapeleka watoto wake chuoni (madrassa) ili wapate kumtambua Mola wao na kuacha tabia mbaya, kama vile kuomba omba. Alimhimiza mwanawe kuwajengea uwezo watoto wake na tabia ya kujitegemea katika maisha. Katika hili, Shaaban Robert anamtaka mwanawe kushikamana na elimu kwa sababu ni muangaza kwa siku za usoni kama inavyobainishwa katika beti hizi hapa chini:

| ***Utenzi wa Siraji*** | ***Utenzi wa Adili*** |
|---|---|
| **47**. Wenu wana wa chuoni<br>Kabisa siliwacheni<br>Wakiomba majumbani<br>Kuomba watazoea | **49.** Maisha bila elimu<br>Hayafai mwanadamu<br>Sababu mambo magumu<br>Mengi sana mbelee |

Taswira ya kusoma katika beti hizi inamtaka msomi kutoziacha kweli za maisha zinazoikabili jamii. Hii ni sawa na kusema kuwa ni wajibu wa kila mwanajamii kuwa na elimu au ujuzi wa maarifa fulani (Mdee, Njogu na Shafi, 2011) muhimu katika maisha. Pamoja na malengo ya makala hii, beti hizi zinaonesha kwamba jamii ya watunzi wateule ilikuwa na elimu zake, kuanzia elimu ya ufunuo (Timammy na Swalehe, 2013), elimu ya ndoa na kazi za kujikumu (Sengo, 1992), na huo ndio mchango husika katika dunia (Mwinyi, 2020).

**5.5 Uvumilivu**

Katika dhamira hii, Kijumwa anamtaka mwanawe avumilie mambo ya kheri na shari zitakazomsibu duniani. Aidha, anamsihi kupunguza hasira na kutosikitika iwapo mambo ya dunia yatamzonga kwani sio dawa. Badala yake, awe na subira pamoja na kumuomba Mungu amtatulie matatizo yake. Naye Shaaban Robert anamtaka mwanawe kudhibiti hasira kwa kujifanya bubu ili kuepusha shari inayoweza kutokea. Hili ni sawa na kusema ukimya ni tabibu na dawa ya jeuri ni *skut*. Beti zifuatazo ni muhimu kuzingatiwa:

| *Utenzi wa Siraji* | *Utenzi wa Adili* |
|---|---|
| 97. Mambo yakikuzingia | 47. Ukiwa na ghadhabu |
| Nyumbani huna rupia | Jifanye kama bubu |
| Wata hasira kungia | Kimya ni utabibu |
| **Na zitunu kuzitia** | Wa hasira uelewe |

Maelezo katika beti hizi yanabainisha kwamba uvumilivu na subira ni silaha za tunu mja kuwa nazo. Kwa maana hiyo, beti hizi zinaonesha hitaji la uvumilivu na subira katika malezi ili wenye kulelewa wapate fursa ya kuelewa maana ya maisha, kupata na kukosa, faida na hasara za hasira katika kukabiliana na tata za maisha. Katika beti hizi, Kijumwa na Shaaban Robert wanatoa funzo kuwa maisha yanahitaji subira, umakini, utiifu na kushirikisha akili na mawazo ya mtu binafsi. Kinyume chake, chambilecho Sengo (2012) na Mwinyi (2020) itakuwa vigumu kwa mtu kupevusha mawazo na kujenga uvumilivu wa moyo unaohitajika maishani.

**5.6 Uadilifu katika Ushahidi**

Katika dhamira hii, Kijumwa anamuusia mwanawe kushikamana na uadilifu katika utoaji wa ushahidi. Hapa, amemtaka kutoa ushahidi kwa analolijua na kutopindisha ukweli kwa jambo asilolijua hata kama atapewa pesa au kuahidiwa utajiri, kama inavyoelezwa:

| *Utenzi wa Siraji* | |
|---|---|
| 26. Swahibu kapatikana | 27. Kuwa shahidi wazuri |
| kenda kushitakiana | Hata kwa nduyo sikiri |
| Uyualo baba nena | Kakupa fedha johari |
| **Usiyua kimbia** | Ni kheri kutopokea |

Katika beti hizi Kijumwa anamfunza mtoto wake uadilifu ambao ni moja ya tunu adhimu za maisha ya watu wenye kujitambua na kutambua lengo lao la maisha.

Pamoja na hili, Sengo (2008) anasema, mafunzo ya awali yanayotolewa na mafundi wa Kiafrika yana maana na thamani kubwa. Yaani, kwa kumfundisha mwanawe uadilifu kwa maana ya kila kitu kukiweka mahali pake stahiki, Kijumwa alichukua nafasi yake kuelekeza maarifa halisi ya kuishi. Katika hoja hii, Shaaban Robert hakuzungumza kitu kinachofanana na Kijumwa.

**5.7 Kutunza Siri**

Hapa Kijumwa na Shaaban Robert wanawataka watoto wao kutunza siri walizoaminiwa na kutozitangaza kwa wasiohusika. Aidha, wamewataka wasizitangaze hata siri zao binafsi kwa adui, ila kwa watu wanaowaamini, kama inavyoelezwa katika beti hizi:

| ***Utenzi wa Siraji*** | ***Utenzi wa Adili*** |
|---|---|
| 103. Waloambiwa kwa siri<br>Usieleze dhahiri<br>Mwenyewe yatamuhairi<br>Kwa faragha humwambia | 77. Hadhari usiiwache<br>Siri yako ifiche<br>Ila watu wachache<br>Wapasao wajuwe |

Matokeo mengine yanayoibuliwa na makala hii ni somo la kutunza siri. Kwa usahihi kabisa, Kijumwa na Shaaban Robert wanawaelekeza watoto katika mahitaji rasmi ya maisha ya tahadhari. Huo ndio Uafrika ambao kwa mujibu wa Kiango na Sengo (1974) na Sengo na Bathawab (2007) ni mfumo wa fikra unaozingatia thamani ya kutunza siri kuu za jamii ili kujenga mitazamo yenye kuheshimu tabia, mila na desturi za Kiafrika kila izungumziwapo fasihi na maisha kwa ujumla. Kwa maana hii, watunzi husika wanawafunza watoto wao kujenga uwezo wa ndani wa kuhifadhi siri ili kuisalimisha jamii dhidi ya mashaka ya kutokuwa na siri. Wazee wa zamani walisema, ‘msimkaribishe mpayukaji katika mawindo mtakosa kitoweo’. Hivyo, kutunza siri kwa mantiki ya watunzi husika ni funzo lenye thamani kubwa ya kuendelea kwa wenye kutafakari.

**5.8 Kutimiza Ahadi**

Shaaban Robert anamuasa mwanawe kutovunja ahadi, isipokuwa ikiwa ni ahadi batili. Mtunzi huyu alimhadharisha kijana wake kuwa, kuacha kutekeleza ahadi kutamvunjia heshima na kumkosesha bahati. Aidha, Shaaban Robert alimtaka mwanawe kuipima ahadi kabla ya kuitamka.

| ***Utenzi wa Adili*** | |
|---|---|
| 78. Na ukiiweka ahadi<br>Kutimiza jitahidi<br>Inabatilisha sudi<br>Ahadi kwa avunjae | 79. Ahadi ni heshima<br>Kabla ya kuisema<br>Wajibu ni kuipima<br>Ndipo kinywani utoe |

Katika beti hizi kuna mafunzo ya kuzingatia. Mosi, Shaaban Robert amemfunza mwanawe muunganiko wa kutunza ahadi na heshima ya mtu. Yaani, somo la kutunza ahadi ni lazima lianzie nyumbani ili kutoa wasaa wa kumwendeleza mtoto au watoto kuliishi hata baada ya kuingia katika jamii pana inayowazunguka. Hapa, mzazi huwa amemsalimisha mtoto (Sengo, 2008). Pili, funzo la kutunza ahadi linaloanzia nyumbani, hutoa fursa ya mzazi kuwa mwalimu wa kwanza mwenye athari kwa mtoto au watoto husika. Athari hizo zinaweza kuwa za kiakili, kiroho, kisaikolojia na kimwili. Katika hoja hii hata hivyo, Kijumwa hakuzungumzia kitu kinachofanana na kilichousiwa na Shaaban Robert. Kwa pamoja, inaweza kusema kuwa watunzi husika waliwafunza watoto wao ili kuacha athari chanya katika jamii zao.

## 6.0 Mjadala wa Ulinganisho wa Dhamira ya Malezi ya Watunzi wa Kiume

Kimsingi, matokeo yanaonesha kuwa watunzi teule wa kiume wamefanana kwa kiasi kikubwa na kutofautiana kwa kiwango kidogo. Watunzi wote wamezungumzia utiifu na heshima, mapenzi na ndoa, bidii katika kazi, elimu ya kujitegemea, uvumilivu na kutunza siri. Wameachana katika hoja ya uadilifu katika ushahidi na kutimiza ahadi. Mathalani, katika kuzungumzia maisha ya Kiislamu, watunzi hawa, kama ilivyokuwa kwa watunzi teule wa kike, waliweka usoni suala la kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu (Mwinyi, 2020). Kufanana huku kumeendana na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kwamba, uhusiano wa kazi za fasihi ni lazima ufanane na muktadha wa jamii zinamoibukia (Wellek na Warren, 1978). Kwa kuwa watunzi hawa ni zao la jamii ya Pwani, ni wazi utunzi wao ulizingatia ukweli kuhusu malezi na makuzi ya vijana na mabinti wa jamii husika (Gibe, 1978). Kwa msingi huu, ndiyo maana waliweza kulinda maadili na falsafa njema za maisha zilizotamalaki katika jamii waliyomo (Mlacha, 1985).

Vilevile, watunzi wateule wa kiume wamejikita zaidi kuwausia watoto wa kiume, ijapokuwa Kijumwa katika suala la ndoa alimgusia pia mtoto wa kike. Ufanano huu unathibitisha hoja kuu ya Nadharia ya Mwingilianomatini kwamba kuna mwingiliano wa matini ya kifasihi na matini tangulizi bila kujali mpishano wa zama (Kristeva, 1966). Kinachotokea ni kazi tangulizi kuweka mwega (Wamitila, 2003), kwa maana ya msingi kwa kazi tangulizi. Pamoja na hilo, hoja hii inaweza kutafsiriwa kwamba mama katika nyumba ana jukumu kubwa la kufunza maadili kwa wanafamilia (Mwinyi, 2020), huku baba akisimamia yote yanayolenga ustawi wa kizazi cha jamii nzima. Kwa mfano, Kijumwa alipomweleza mwanawe achague ukoo wenye nasaba ya kutambulikana ili naye atambulike na kumnasihi kutofanya ajizi ya kutoa talaka mara tu mke anapoidai. Hii inaonesha kwamba, Kijumwa alijeruhiwa ndani ya ndoa yake na hakupendelea mwanawe yaje yamfike. Tofauti na mtazamo wa Kijumwa, Sengo (1992) ana hoja kwamba ndoa ni asasi muhimu kwa watu wa asili ya pwani ya Afrika Mashariki.

Hivyo, matatizo katika ndoa hukabiliwa kwa juhudi za kuleta maelewano kwanza kabla ya kuivunja. Kimsingi, mwingiliano wa matini wa kazi za Kijumwa na Shaaban Robert unaafikiana na mtazamo wa Nadharia ya Mwingilianomatini, na pia unatoa mchango muhimu, ambao kwa mujibu wa Gibe (1978) unaonesha namna watunzi wa kazi za fasihi wanavyoweza kutumia elimu yao kusaidia jamii kwa kuyazungumza yanayowahusu wanajamii husika. Kwa pamoja, mpishano wa dhima za Kijumwa na Shaaban Robert unaweza kuelezwa kuwa ni matokeo ya uzoefu tofauti wa maisha na mazingira walimokulia watunzi wawili hao.

## 7.0 Kulinganisha na Kulinganua Dhamira ya Malezi baina ya Watunzi wa Kike na Kiume

Imesadifu kuwa watunzi wote wanne tuliowateua ni waumini wa dini ya Kiislamu, hili hatukuweza kulikwepa. Kutokana na hilo, kumekuwa na kulingana kwa kiasi kikubwa katika kuyaelezea malezi. Kwa muktadha wa lengo hili, dhima ya kumcha Mwenyezi Mungu na uwazi wa mafunzo kuhusu maisha ya ndoa ziliibuka kama ifuatavyo:

### 7.1 Kumcha Mwenyezi Mungu

Katika dhima hii, watunzi teule wote wa kike na kiume wameonesha mfungamano mkubwa wa kuhimiza mahusiano baina ya viumbe na Mola wao na viumbe kwa viumbe kama msingi madhubuti wa malezi yenye tija. Kwa mujibu wa Mwinyi (2020), inaweza kusemwa kuwa taamuli ya imani ya Mwenyezi Mungu ni msingi katika malezi katika jamii ya pwani. Watunzi teule wameliishi hili kwa kuamini kuwa imani ya wanajamii ni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye mlezi. Kwa kufanya hivyo wamenasibu na Nadharia ya Sososholojia ya Fasihi kama ilivyofafanuliwa na Wellek na Warren (1978). Hata hivyo, tofauti ndogo iliyojitokeza baina ya wazazi hawa ni hisia za mama katika malezi. Mwanakupona na Zaynab walitumia lugha ya upole na ukarimu, yenye kushawishi, kubembeleza, kuliwaza na kufunza (Hamad, 2016). Ukilinganisha na Kijumwa na Shaaban Robert, ambao yamkini kutokana na kuchukua muda mrefu katika kusaka chajio (Kombo na Kipacha, 2009) hawakuwa na muda wa kutosha wa kukaa na watoto wao kuwafundisha.

### 7.2 Msisitizo wa Maadili katika Maisha ya Ndoa

Dhima nyingine iliyoibuliwa na watunzi hawa ni msisitizo wa maadili katika maisha ya ndoa. Kwa pamoja, watunzi husika wa kike wamekuwa wawazi mno katika kuyaeleza masuala ya ndoa kwa binti zao kuliko watunzi wa kiume kwa vijana wao. Kwa mujibu wa Mwinyi (2020), maadili kwa wanandoa ni tunu isiyokonga, na ndiyo hali tuliyo nayo wanadamu (Sengo, 2007). Katika sehemu nyingine, Njozi (1990) na Sengo (2007) wanaweka wazi kuwa kwa sababu ya mila na desturi za jamii ya pwani, mambo ya ndani ya ndoa ni jukumu la wanawake wajuzi katika jamii za pwani na za Kiafrika kwa ujumla wake. Hizo ndizo mila na desturi za Waswahili (Njozi, 1990). Kwa mintarafu ya lengo hili inaweza kusemwa kwamba watunzi wa kazi za fasihi wana jukumu kubwa la kutunga na

kuakisi muktadha wa jamii zao. Vilevile, wasomaji na wahakiki wanatarajiwa wafanye jitihada kuwaelewa watunzi kwa mantiki na muktadha wanamoandikia ili kupata ujumbe unaotekelezeka.

**8.0 Dhima za Tenzi Teule Kifasihi, Kijamii na kwa Watunzi wenyewe**

Tenzi zilizochunguzwa zina dhima tofauti kifasihi, kijamii na kwa watunzi wenyewe kama zilivyodhihirika na kuelezwa ifuatavyo:

**8.1 Mazingatio ya Muktadha wa Jamii**

Kifasihi, tenzi teule zimeonesha haja ya kuzingatia muktadha wa jamii husika katika kuibua, kujadili na kufikisha ujumbe kwa hadhira. Lengo ni kuepuka mchujuko wa kazi husika ndani ya kipindi kifupi. Kimsingi, jambo hili linaweza kufanywa kwa watunzi kujikita katika kuheshimu misingi na mikondo mizuri ya jamii wanazoziandikia (Mwinyi, 2020). Pia, jambo hilo linaweza kufanywa kwa kuzingatia hifadhi na maendeleo mema ya hadhi na taadhima ya maisha (Sengo na Kiango, 1973). Kwa upande wao, wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi wanatarajiwa kuongeza jitihada za kuwaelewa watunzi kama Mwanakupona au Zaynab, kwa mantiki waliyoyakusudia na muktadha lengwa. Pengine, ni kutokana na aina hii ya mtazamo, ndipo Njozi (1990) aliposema kuwa wanaomjadili Mwanakupona kwa jicho la ukandamizaji wa mwanamke hawakumuelewa. Hapa, ndipo inapoonekana haja ya kuzingatia Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi, inayokuwa kiunzi cha kuongoza uandishi na uhakiki wa kazi za fasihi (Gibbe, 1997). Hivyo basi, ni muhimu watunzi pamoja na wahakiki kuvaa viatu vya jamii husika ili kupata undani wa kinachokusudiwa.

**8.2 Nafasi ya Baba na Mama katika Malezi**

Kijamii, tenzi tajwa zimetoa picha halisi kuhusu nafasi ya baba na mama katika kulea watoto kwa mazingatio ya amali na tunu zake. Chambilecho Mwinyi (2020), baba na mama wanapohitimishana katika ndoa hujenga mapenzi ya watoto. Kinyume chake, baba na mama wanapohasimiana, watoto husambaratika. Inaweza kusemwa kuwa, watunzi teule kwa umahiri mkubwa, kama alivyopata kubainisha El-Maawy (2011) wameonesha thamani ya ulezi wa roho na mwili ambao ndani yake hutoa fursa ya kukamilishana na kupata mtu kamili. Kwa muktadha wa Nadharia ya Mwingilianomatini, tofauti ya zama za akina Mwanakupona na Zaynab na Kijumwa na Shaaban Robert hazikuwa kikwazo. Bado akina Zaynab na Shaaban Robert wameendelea kupata mwega wa kuzingatia na kusimamia kufikisha ujumbe walioukusudia kama ulivyofikishwa na akina Mwanakupona na Kijumwa. Hivyo, kwa makala hii tunaweza kusema kwamba malezi ya pamoja ya baba na mama hujenga mapenzi kwa watoto.

### 8.3 Ukamilifu katika Malezi

Kwa watunzi wenyewe, tenzi teule zinaonesha thamani na uzito wa kulizungumza jambo kwa mapana yake. Mathalani, malezi ya kiroho, kiakili na kiwiliwili yamejitokeza kuwa ni jambo lililowashughulisha watunzi wote. Kitu kikubwa kilichojitokeza ni kwamba kwa wanajamii wa pwani ambako ndiko watunzi teule walikoishi, imani kwamba Mwenyezi Mungu ndiye mlezi limejitokeza kwa uzito mkubwa. Hapana shaka, kwa jamii husika imani hiyo ndiyo inayohitajika kupata ukamilifu wa malezi bora ya watoto (El-Maawy, 2012), ambalo ni jambo la kila siku na kila wakati ndani ya jamii lengwa (Mwinyi, 2020). Kwa mintarafu ya lengo hili, inaweza kusemwa kuwa ukamilifu wa malezi ni pamoja na kuzingatia kweli za kiroho, kiakili na kimwili kwa anayelelewa ili kupata mafanikio ya duniani na akhera. Msingi wa malezi hayo ni ndoa halali ya mume na mke, ambayo Timmmy na Swalehe (2013) wanasema ni utekelezaji muhimu wa dini na ni msingi wa kupata raha ya dunia na akhera.

## 9.0 Hitimisho

Kiuchunguzi, tunakiri kuwa fasihi haitoki katika ombwe bali ni zao la jamii ya mwandishi. Kwa kuzingatia malengo ya makala hii, inaweza kuhitimishwa kuwa imani kwa Mwenyezi Mungu ni msingi mkuu katika malezi. Abdallah (2011) anasema fasihi ya maana ni lazima itokane na hali halisi ya jamii inayozungumzwa. Msingi wa hoja ni kuwa maudhui hayapaswi kujitenga kuzungumzia maisha ya jamii husika. Ndivyo walivyofanya akina Kijumwa, Shaaban Robert, Mwanakupona na Zaynab katika kazi zao teule. Aidha, wazazi wote wana jukumu la kufanya kazi kwa pamoja kuwalea watoto katika maadili yanayofaa. Pia, tofauti ya zama si kikwazo cha kupata mwega kwa watunzi kutunga kazi za fasihi zisizochuja. Hapa, ni sawa na kusema ya kale ni dhahabu, kwa maana kizazi kipya cha watunzi kina dhima ya kujifunza kwa akina Zaynab na Shaaban Robert, hususani namna walivyofaidika na kazi za watangulizi wao.

## 10. Mapendekezo

Wazazi na walezi katika zama za kidijiti wanawajibika kulea watoto wao kwa mujibu wa taratibu za jamii zao. Kwa pamoja, mtazamo wa malezi ya watunzi wateule una nafasi katika zama za sasa kwa jamii zenye ghera ya mustakabali mwema kwa watu wake. Kwa pamoja, dhima ya malezi inahitaji kufanyiwa kazi na makundi yote ya watu katika jamii, bila ya kujali tofauti ya zama ili kuwa na ustawi mzuri wa jamii ya mwanadamu.

## Marejeleo

Abdalla, A. (2011). “Utangulizi wa Mhariri.” Katika A. Abdalla (Mh.), *Kale ya Washairi wa Pemba: Kamange na Sarahani*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers. Kur. xxvii-xxviii.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Boell, S.K. na Cecez-Kecmanovic, D. (2014). "A Hermeneutic Approach for Conducting Literature Reviews and Literature Searches." *Communications of the Association for Information Systems*. 34(1): 12.

Cohen, L., Manion, L. na Morrison, K. (2011). *Research Methods in Education* (Toleo 7). London: Routledge.

Egl, M.I. (1983).*The Life and Works of Muhamadi Kijumwa*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha London.

El-Maawy, A. (2011). *Jawabu la Mwana Kupona: Mausiyo ya Mke wa Kisasa na Waasiya wa Mwanakupona*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Gibbe, A. (1993). *Women and the Making of Literature in East Africa*. OSSREA 4th Gender Issue Competition. (Muswada ambao haujachapishwa).

Hamad, A. (2016). "Utandawazi katika Utamaduni wa Vijana wa Kizanzibari." *Jahazi*. 1: 1-16.

Khamis, A. (2016). "Utandawazi katika Utamaduni wa Vijana wa Kizanzibari." *Jahazi*. 1: 1-16.

Khatib, M. (1985). "Utenzi wa Mwanakupona." *Mulika*. 17: 46-52.

Kijumwa, M. (1927). *Utendi wa Siraji*. Maktaba ya Lamu Fort. (Haujachapishwa).

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Litrature and Art.* NewYork:
Columbia University Press.

Maina, V. (2005). *Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert*: *Utenzi wa Hati* na *Utenzi wa Adili*. Tasnifu ya Uzamahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J. (2015). *African Religious and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mdee, J. na Wenzake (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mlacha, S.A.K. (1995). "Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba". Katika S.A.K. Mlacha na A. Hurskainen (Wah.), *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 16 - 26.

Mulokozi, M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mwinyi, M. (2020). *Kilingo cha Utenzi wa Mwanakupona katika Usawiri wa Mwanamke wa Pwani: Mifano kutoka Kisiwa cha Tumbatu na Lamu*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ndalu, A.E., Babusa, H. na Mirikau, S.A. (2014). *Kamusi Teule ya Kiswahili: Kilele cha Lugha*.
Nairobi: East African Educational Publishers.

Njozi, H. (1990). "Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics". *Kiswahili*. Juz. 57: 55-67.

Othman, S.Y. na Yahya, A. S. (Wah.) (2011). *Howani Mwana Howani*: *Tenzi za Zaynab Himid* Mohammed. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Ponera, A. (2014) *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Robert. S. (1939). *Utenzi wa Vita vya Uhuru.* Nairobi: Oxford University Press.

Robert. S. (1946). *Almasi za Afrika*. Nairobi: Nelson.

Robert. S. (1959). *Kielezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.

Robert. S. (1966). *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.

Robert. S. (1967). *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robert. S. (1969). *Mapenzi Bora*. Nairobi: Nelson.

Sengo, T.S.Y. (1992). Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja. *Nordic Journal of African Studies*. 1(1):53-79.

Sengo, T.S.Y na Kiango, S.D. (1974). *Ndimi Zetu: Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longman.

Sengo, T.S.Y. na Bathawab, S.S.M. (2007). *Utendi wa Mambo Mambo*. Dar es Salaam: Al- Amin Education and Research Academy.

Sengo, T.S.Y. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.

Sengo, T.S.Y. na Kiango, S.D. (2012). *Hisiya Zetu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi*: *Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shitemi, N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Nairobi: Kijabe Printing Press.

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013) "A Thematic Analysis of Utendi wa Mwanakupona: Swahili/Islamic Perspective". *International Journal for Innovation Education and Research*. 4 (8): 9-15.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wellek, R. na Warren, A. (1978). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.